**HOTUBA YA AFISA MTENDAJI MKUU MAMLAKA YA MASOKO YA MITAJI NA DHAMANA (CMSA), CPA. NICODEMUS MKAMA, KWENYE UZINDUZI WA SHINDANO LA MASOKO YA MITAJI KWA WANAFUNZI WA VYUO VIKUU NA TAASISI ZA ELIMU YA JUU (CMUHLIC) 2020; ILIYOFANYIKA KATIKA OFISI ZA MAMLAKA, GHOROFA YA 6 JENGO LA PPF TOWER, TAREHE 4 AGOSTI 2020.**

Uongozi wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA),

Wawakilishi wa Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu,

Washindi wa Shindano la Masoko ya Mitaji kwa Wanafunzi wa Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu wa Mwaka Uliopita,

Waandishi wa Habari,

Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,

Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kujumuika katika hafla hii ambayo ni ya kihistoria katika sekta ya fedha hapa nchini.

Pili, napenda kuwashukuru wote kwa kuweza kutenga muda kutoka kwenye ratiba zenu zenye majukumu mengi, makubwa, muhimu na kuweza kuhudhuria hafla hii.

Kuhudhuria kwenu hapa, ni uthibitisho wa nia dhahiri mliyonayo ya kushirikiana na Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi madhubuti Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kuweka mazingira bora, shirikishi na endelevu ya kisera, kisheria na kiutendaji yenye lengo la kukuza uwekezaji kwenye sekta ya fedha kupitia masoko ya mitaji na hivyo kuchochea ukuaji na maendeleo ya uchumi hapa nchini.

**Ndugu Wageni Waalikwa,** Masoko ya mitaji ni sehemu ya mfumo wa sekta ya fedha inayowezesha upatikanaji wa fedha za muda mrefu, yaani zaidi ya mwaka mmoja, kwa ajili ya kugharamia shughuli za maendeleo. Fedha za kugharamia shughuli za maendeleo hupatikana kwa kuuza hisa za kampuni (shares), hatifungani za kampuni (corporate bonds), hatifungani za Serikali (Government bonds) na vipande katika uwekezaji wa pamoja (collective investment schemes). Masoko ya mitaji ni muhimu katika

kuchochea maendeleo na ukuaji wa uchumi kwa kuwa huwezesha fedha kupatikana kutoka kwa watu binafsi, taasisi, kampuni na hatimaye huwekezwa katika sekta ya uzalishaji na kutekeleza miradi ya maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30 Julai 2020 uwekezaji katika masoko ya mitaji una thamani ya jumla ya Shilingi Trillioni 27.04 ambapo uwekezaji kwenye hisa ni Shilingi Trillioni 15.19; Hatifungani za Serikali Shilingi Trillioni 11.28; Hati Fungani za Kampuni Shilingi Billion 176.04; na mifuko ya uwekezaji wa pamoja Shillingi billion 378.93.

**Ndugu Wageni Waalikwa**, Masoko ya Mitaji hapa nchini yanasimamiwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA). Pamoja na jukumu la kusimamia Masoko ya mitaji, CMSA pia ina jukumu la kujenga uwezo na kutoa elimu kwa umma juu ya fursa na faida za kuwekeza katika masoko ya mitaji na kukuza uchumi. Katika jitihada za kutekeleza jukumu hilo, Mamlaka, leo inazindua Shindano kwa Wanafunzi wa Vyuo vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu (**Yaani** the Capital Markets Universities and Other Higher Learning Institutions Challenge) kuhusu kujenga uelewa na ueledi wa uwekezaji katika masoko ya mitaji, kwa kutumia teknojia ya mitandao ya kielektroniki yaani simu za mikononi na intaneti. Shindano hili llinafunguliwa leo tarehe

04 Agosti na litahitimishwa tarehe 31 Oktoba 2020. Shindano hili limegawanyika katika sehemu kuu mbili, ambazo ni (shindano la maswali na majibu - Quiz Competition) na (Shindano la kuandika Insha - Essay Competition).

**Shindano la kwanza la Maswali na Majibu (Quiz Competition),**

Kupitia shindano hili, wanafunzi wanatakiwa kujibu maswali 100 kwa kutumia simu za mkononi, ambapo mshiriki anatakiwa kujisajili kwa kuandika majina matatu; jinsia; chuo; na kozi anayosoma, na kisha kutuma ujumbe mfupi wa maandishi kwenda namba 0766 046046.

**Shindano la pili la Kuandika Insha (Essay Competition),**

Kupitia shindano hili, wanafunzi wanatakiwa kuandika insha kuhusu "*Fursa na Manufaa ya Uwekezaji Katika Masoko ya Maitaji"* kwa kutoa mifano halisi. Insha hiyo inatakiwa isizidi kurasa nne (4), maneno 1,500 na kisha kuituma insha hiyo kwenye barua pepe ambayo ni challenge@cmsa.go.tz.

Washindi katika mashindano haya ni wale ambao watapata alama za juu kuliko washiriki wengine na ambao wataweza kujibu kwa ufasaha maswali ya usaili utakaofanyika mbele ya jopo la majaji na kudhihirisha kuwa wao ni washindi katika hafla ambayo itafanyika kwa uwazi na kushuhudiwa mubashara na umma wa watanzania katika redio na televisheni.

**Wageni Waalikwa**, CMSA imelenga kuwafikia angalau Wasomi wa Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu wapatao 60,000 wawe wamepata elimu ya masoko ya mitaji ifikapo mwishoni wa mwaka 2020. Hadi sasa tumefikia wanafunzi 48, 680 na tuna lengo la kuwafikia wanafunzi 16,000 katika

shindano la mwaka huu. Ni matumaini yetu tutaweza kuvuka lengo la kupata washiriki 60,000 ifikapo mwisho wa mwaka huu. Kwa mantiki hiyo natoa wito kwa wanavyuo kujitokeza kwa wingi na kushiriki katika shindano hili kwani linatoa fursa mbali mbali sio tuu kwa zawadi zitakazoshindaniwa bali fursa za uwekezaji na ajira ambazo zitachangia kukuza kipato cha mtu mmoja mmoja na hivyo kuleta matokeo chanya katika katika kujenga na kuendeleza uchumi wa mtu binafsi na uchumi wa nchi kwa ujumla.

**Wageni waalikwa**, Hafla ya leo inaweka historia kubwa sio tu katika maendeleo ya masoko ya mitaji hapa nchini, bali pia katika ukanda wa Afrika Mashariki kwani tangu shindano hili lilipofunguliwa limeweka historia mpya katika sekta ya masoko ya mitaji kwa kuwa shindano la kwanza kuhusu masoko ya mitaji kwa wanafunzi wa vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu katika ukanda wa Afrika ya Mashariki na Kusini mwa bara la Afrika, ambalo limehusisha teknolojia ya mawasiliano ya mtandao kwa njia ya simu za mkononi. Shindano hili, limeweza kuvutia Mamlaka za Masoko ya Mitaji za Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika kuja nchini kujifunza jinsi ya kuendesha mashindano kama haya katika nchi zao.

**Wageni Waalikwa,** katika jitihada za kukuza na kuendeleza masoko ya mitaji hapa nchini, Mamlaka imeweka mpango mkakati wa kuwawezesha washiriki wa shindano hili kuwa wawekezaji halisi. Hatua hii inalengo la kuwezesha kutumia nadharia kwa vitendo elimu ambayo washiriki hawa wanaipata kupitia shindano hili. Kupitia mpango huu wanafunzi wapatao 350 wameweza kuwekeza kwenye masoko ya mitaji kwa kununua hisa za Kampuni mbalimbali zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam.

**Wageni Waalikwa**, washindi wa shindano watapata zawadi zifuatazo:

a) Washindi wa kwanza kwa kila shindano kwa upande wa wavulana na wasichana watapata shillingi milioni moja na laki nane (TSH 1,800,000);
b) Washindi wa pili kwa kila shindano kwa upande wa wavulana na wasichana watapata shillingi milioni moja na laki nne (TSH 1,400,000);
c) Washindi wa tatu kwa kila shindano kwa upande wa wavulana na wasichana watapata shillingi laki nane (TSH 800,000);
d) Washindi wa nne kwa kila shindano kwa upande wa wavulana na wasichana watapata shillingi laki nne (TSH 400,000);
e) Washiriki waliobaki katika kumi bora watazawadia shilingi laki mbili (TSH 200,000
f) Washiriki wote waliofika fainali na kuwa miongoni mwa washindi 20 walioshika nafasi za juu watapatiwa vyeti (certificate of recognition); fulana; na kofia zenye nembo ya Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana; na
g) Washiriki 6 wavulana; na 6 wasichana wenye alama za juu zaidi watagharamiwa ziara ya kutembelea maeneo mbalimbali ili kujifunza zaidi masuala ya masoko ya mitaji ikiwa ni pamoja na masoko ya hisa na kampuni kubwa zinazohusika na utoaji huduma katika masoko ya mitaji.

**Wageni waalikwa,** Tunatarajia kwamba ziara hii ya mafunzo itasaidia kujenga ujuzi wa washiriki katika masoko ya mitaji na washindi hao watakuwa mabalozi bora wa masuala ya masoko ya mitaji kwa wanafunzi

wengine, kwa kutoa elimu na ujuzi kwa wanafunzi katika vyuo vikuu; taasisi za elimu ya juu; na umma kwa ujumla, kwani wanafunzi waliopatiwa mafunzo kama haya katika shindano lililopita wamepata fursa ya kufanya kazi katika kampuni kubwa za Kimataifa zinazotoa huduma za ushauri katika masuala ya fedha, kodi na uwekezaj. Kampuni hizo ni pamoja na Price Waterhouse Coopers (PWC), KPMG, Deloitte & Touche, Ernest & Young; pamoja na baadhi ya Benki na kampuni zenye leseni kutoka CMSA. Aidha baadhi yao wameanzisha kampuni ambazo tayari zimekwisha pata leseni ya kutoa huduma katika masoko ya mitaji. Kampuni hizo ni pamoja na Beacon Financial Services, ambayo Afisa Mtendaji Mkuu wake ni Miongoni mwa wanafunzi ambao wamekwisha fuzu mafunzo ya watendaji katika masoko ya Mitaji wanaokidhi viwango vya kimataifa.

**Ndugu Wageni Waalikwa,** pia hapa tunao baadhi ya wanafunzi washindi wa shindano la mwaka jana ambao wameweza kuendeleza ndoto zao za kushiriki kwenye soko la hisa na hivyo kutumia sehemu ya fedha zao walizopata kama zawadi kununua hisa za kampuni mbalimbali zilizoorodheshwa katika Soko la Hisa. Hawa sasa wamekuwa wawekezaji halisi na sio kwa kusoma tu. Hawa pia, leo utawakabidhi vyeti vya umiliki wa hisa zao walizonunua kwa fedha za zawadi ya ushindi na wengine wameongezea fedha zaidi ya hizo na kununua hisa. Natoa rai kwa washindi wa mwaka huu kuiga mfano huu bora sana wa kuwa wawekezaji halisi katika masoko ya mitaji.

***Ndugu Wageni Waalikwa,*** Kadiri Taifa letu linavyosonga mbele katika utekelezaji wa Sera ya Uchumi wa Viwanda, mahitaji ya fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo hususani miundombinu yanaongezeka. Serikali na kampuni binafsi zinaweza kujipatia fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo kwa njia ya kuuza hisa, hatifungani na bidhaa zingine za masoko ya mitaji. Ili kufanikisha azma hii, kunahitajika kuwepo kwa wawekezaji wengi wenye uelewa na ujuzi katika sekta ya fedha . Hatua hii ni muhimu kwani inachangia kuongezeka kwa uwekezaji na hivyo kuchochea ukuaji wa Uchumi wa Viwanda hapa nchini. Hivyo basi, mkakati huu unatekelezwa katika wakati muafaka kwani unaunga mkono juhudi madhubuti za Rais wetu mpendwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dr. John Pombe Joseph Magufuli katika kuifanya Tanzania ya viwanda na uchumi wa kati ambao ni endelevu.

Baada ya kusema hayo napenda kutamka rasmi ya kuwa shindano la masoko ya mitaji kwa wanafunzi wa vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu Tanzania kwa mwaka 2020 limezinduliwa rasmi.

**Mungu Ibariki Tanzania, Asanteni sana kwa kushiriki kwenu**